

**Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Dkt Doroth Gwajima akizungumza na wazee katika Kijiji cha Sukamaela Wilayani Manyoni.**

Imewekwa mtandaoni

6 September 2021

Waziri wa Afya, Maendeleoa ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto Dkt. Dorothy Gwajima,Amesema kuwa SERIKALI ipo katika hatua za mwisho za mapitio ya Sera ya Wazee ya mwaka 2003, ikiwa ni hatua ya kutimiza azma ya kuimarisha afua mbalimbali kwa wazee nchini.

Hayo yamesemwa leo katika kijiji cha Sukamahela Wilayani Manyoni wakati akitoa taarifa kwa umma kuhusu maadhimisho ya siku ya kimataifa ya Wazee Duniani Okotoba 1.

Dkt. Gwajima amesema masuala mbambali katika sera hiyo ikiwemo huduma za Afya, matunzo, ulinzi na usalama, hifadhi ya jamii, maandalizi ya wananchi kuelekea maisha ya uzee na msaada wa kisaikolojia yamewekewa mikakati madhubuti ili kuhakikisha wazee wanapata huduma jumuishi na stahiki kwa ajili ya ustawi na maendeleo yao.

"Vilevile Serikali kwa kushirikiana na wadau imeendelea kutekeleza afua mbalimbali zinazalenga katika kutatua changamoto mbalimbali zinazaowakabili wazee"alisema Dkt. Gwajima

Aidha amesema kuwa  sherehe za maadhimisho ya siku ya wazee mwaka huu zitaambatana na huduma mbalimbali ikiwemo kupimwa maradhi mbalimbali kama vile presha, kisukari na tezi dume.

Dkt. Gwajima ameongeza kuwa zitatolewa huduma za msaada wa kisaikolojia na elimu kuhusu kujikinga na ugonjwa wa UVIKO-19 pamoja na kuhamasisha wazee na wananchi kupata chanjo.

"Halikadhalika kuelekea siku ya kilele cha maadhimisho hayo mwaka huu nchini wazee watapata fursa ya kukutana na kujadili mambo mbalimbali yanayohusu maisha yao na kuweka mapendekezo ya namna bora ya kushughulikia changamoto zinazowakabili"alisema Dkt. Gwajima

Amesema lengo la maadhimisho hayo ni kuongeza uelewa wa jamii kuhusu masuala mbambalimbali ya wazee ikiwa ni pamoja na kutafakari fursa na changamoto zinazo wakabili na namna ya kuzitatua.

"Hivyo ni wajibu wetu kama taifa kutumia siku hii kutambua machango wa wazee na kuwaenzi ipasavyo kwa kulinda, kuhifadhi, kukuza na kuimarisha upatikanaji wa haki zao katika jamii"alisisitiza Dkt. Gwajima

Kadhalika amesema maadhimisho hayo yatafanyika katika ngazi za mikoa na maeelekezo tayari yametolewa kupitia Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI.

“Kauli mbiu ya maadhimisho kwa mwaka huu inasema ‘Matumizi sahihi ya kidigitali kwa ustawi wa rika zote’ujumbe huu umewekwa mahususi ili kusisitiza umuhimu wa kutoa nafasi kwa wazee kushiriki katika matumizi ya kidigitali ili kutatua changamoto mbalimbali na kufanya shughuli za ubunifu katika kujiletea maendeleo”alisema Dkt Gwajima.

Amesema taarifa ya umoja wa Mataifa katika masula ya Mawasilinano ya mwaka 2019, inaonyesha kuwa wanawake na wazee ndio makundi ambayo yameachwa nyuma katika matumizi ya digitali.

Aidha ameupongeza Uongozi wa Wilaya ya Manyoni chini ya Mkuu wa Wilaya Rahabu Mwagisa ,Mkurugenzi wa Halmashauri Melkzedek Humbe na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Wilaya ya Manyoni Dkt Furaha Mwakafwila kwa jinsi ambavyo wameonyesha kujali kusimamia na kuhakikisha huduma zinazotolewa katika Zahanati ya Sukamahela inakidhi haja ya Wazee katika Kijiji hicho.

“Nimefurahishwa sana na huduma za hapa kwani nimeona zinakidhi haja ya wazee waliopo hapa mbali na kwamba wanakijiji wengine wanapata huduma lakini mmeelekeza huduma kwa wazee hawa”amesema Dkt Gwajima.



**Waziri wa afya maendeleo ya jamii jinsia wazee na watoto Dkt Doroth Gwajima akikagua bustani ya mbogamboga inayosimamiwa na kikundi cha mapambuzuko kilichoko chini ya wazee wanaoishi katika kituo cha wazee sukamahela**




**Waziri wa Afya maendeleo ya jamii jinsia, wazee na Watoto Dkt Doroth Gwajima akiongea na mzee ambaye ni miongoni mwa wazee wanaoishi katika kituo cha wazee Sukamahela**



**Waziri wa Afya maendeleo ya jamii jinsia, wazee na Watoto Dkt Doroth Gwajima akelekea ndani ya nyumba mojawapo wanazoishi wazee katika kituo cha wazee sukamahela**


**Mganga Mkuu wa Wilaya ya Manyoni Dkt Furaha Mwakafwila akipokea maelekezo kutoka kwa Waziri wa afya maendeleo ya jamii, jinsia, wazee na watoto**



**Waziri wa afya , maendeleo ya jamii jinsia, wazee na Watoto akikagua huduma ya dawa zipatikano katika zahanati ya sukamahela endapo pia zinakidhi kwa wazee**



**Waziri wa Afya Doroth Gwajima Akijidhirisha na  dawa zitolewazo na Zahanati ya Kijiji cha Sukamahela na kuwapongeza viongozi kwa namna wanavyojali Afya za wazee**



**Waziri wa afya jinsia maendeleo ya jamii wazee na Watoto akimsalimu mtoto ambayea amefika na mama yake katika zahanati ya sukamahela ili kupata matibabu.**



**Waziri wa Afya Doroth Gwajima akikagua Mfumo wa ICHF iliyoboreshwa katika Zahanati ya Kijiji cha Sukamahela**



**Mkuu wa Wilaya ya Manyoni Rahabu Mwagisa akiongozana na Mh Waziri wa Afya jinsia, maendeleo ya jamii ,wazee na Watoto Dkt Doroth Gwajima kuelekea Zahanati ya Sukamahela kuwasalimia wagonjwa mara tu baada ya kumpokea**



**Mkuu wa wilaya ya Manyoni Rahabu Mwagisa akimpokea Mh Waziri wa Afya Mh Waziri wa Afya jinsia, maendeleo ya jamii wazee na Watoto Dkt Doroth Gwajima mara tu alipowasili katika eneo wanapoishi wazee katika Kijiji cha Sukamahela**



**Wazee na wanakijiji wengine waliofika kumsikiliza Mh Waziri Dkt Doroth Gwajima**



**Mkuu wa wilaya ya Manyoni Rahabu Mwagisa akitoa utambulisho wa viongozi aliaoambatana nao**



**Mh Waziri akikagua zizi la mbuzi ambao ni mradi unaoendelezwa na kikundi cha mapambuzuko kinachohudumia wazee Sukamahela**